# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHOMA

**Juni, 2023**

**Igunga – Tabora**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA**

**MKOA WA TABORA**
**WILAYA YA IGUNGA**
**SIMU: 0758933861**

**SHULE YA SEKONDARI CHOMA,**
**S. L. P 222,**
**IGUNGA.**

---

**KUMB. NA. CHSS/J.I/VOL. I/ 1**

NDG. MZAZI/MLEZI WA

______________________________________

______________________________________

YAH: **MAELEKEZO YA MWANAO KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO (V) KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHOMA**

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu.

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao______________________________________ ni miongoni mwa vijana wachache waliopata bahati/fursa ya kuendelea na masomo ya kidato cha tano katika shule ya sekondariCHOMA – Hongera sana.

Kwa barua hii nakuletea fomu ya kujiunga na shule ya sekondari CHOMA kwa mwanao. Tafadhali nakuomba wewe na mwanao msome maelekezo haya kwa kina na kisha mkamilishe yale yote yanayotakiwa.

Pamoja na kuyasoma kwa kina naomba uendelee kumshauri mwanao juu ya kutumia vyema nafasi hii aliyoipataili lengo na azma yake itimie.

Nakutakia maandalizi mema na karibu sana Choma Sekondari.

*KARIBU SANA*

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI CHOMA
S.L.P 222
IGUNGA

William Emidi
Augustine
**MKUU WA SHULE**
**0758933861**

W

**KUMB.NA: CHSS / J. I / VOL. I / 1** **Tarehe: 04 / 06 / 2023**

**MZAZI / MLEZI WA: ____________________________________________**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHOMA KIDATO CHATANO KWA MWAKA WA MASOMO 2023/2024.**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha **Tano** katika **Shule yaSekondari CHOMA, iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Igunga katika Mkoa wa Tabora kwa** mwaka wamasomo **2023 / 2024 kwa TAHASUSI / COMBINATION ya ___________** Nampongeza mwanao kwa kuchaguliwa kwake, akumbuke kwamba hii ni bahati kubwa na ya pekee kwake.

**MAHALI SHULE ILIPO:**

Shule ipo Km. 27 kutoka Ziba kwenye barabara kuu ya lami ya Mwanza - Dar-es-Salaam. Ukifika Choma, Shule ipo Mita 500 tu kutoka kilipo kibao cha Shule (**Sign Block**). Shule hii ni ya mchanganyiko wavulana na wasichana. Wanafunzi wote wa Kidato cha I-IV wanasoma Kutwa, isipokuwa wanafunzi wachache wasichana wanakaa katika Hostel iliyojengwa na wazazi kwa kuzingatia umbali wa watoto wakike wanakotoka.
Wanafunzi wote wa kidato cha V&VI; wanakaa Bweni.

**USAFIRI;**

Usafiri wa kufika Choma Sekondari ni wa Mabasi yaendayo kila siku Igunga Mjini na Nzega Mjini yakiwa yanatokea Choma. Kwa anayetoka Igunga Mjini kuja Choma Nauli ni Tshs. 5,000/= na kwa anayetoka Nzega Mjini kuja Choma Nauli ni Tshs. 4,000/=. Ukishuka Ziba, Nauli ya kuja Choma ni Tshs. 3,000/=
Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **14/08/2023 siku ya jumatatu** hivyo mwanao anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13/08/2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/08/2023 na baada ya tarehe 31/08/2023** nafasi hii ya mwanao atapewa mwanafunzi mwingine mwenye sifa.

Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo ili uzishughulikie haraka na kuzirejesha shuleni mapema iwezekanavyo au siku ya kuripoti Shuleni.

- Fomu Namba 1: Mahitaji ya Shule na Vifaa vya Lazima
- Fomu Namba 2: Taarifa za Mwanafunzi.
- Fomu Namba 3: Taarifa za Mzazi au Mlezi
- Fomu Namba 4: Fomu ya kukubali au kukataa nafasi ya kujiunga na kidato cha tano pamoja na kuzikubali Sheria za Shule.
- Fomu Namba 5: Fomu ya kupima Afya ya Mwanafunzi

# FOMU NAMBA 1.

## A: MAHITAJI YA LAZIMA YA SHULE

### 1.0: MICHANGO MBALI MBALI

**JEDWALI LA UFAFANUZI WA ULIPAJI WA MICHANGO MBALI MBALI YA SHULE;**

| NA | FEDHA KWA AJILI YA | KIASI TSHS |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa shule | Tshs 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | Tshs 5,000/= |
| 3 | Nembo | Tshs 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | Tshs 5,000/= |
| | **JUMLA** | **Tsh 80,000/=** |
| 5 | Fagio la nje | AJE NAVYO |
| 6 | Fagio la ndani.**(Soft Bloom)** + Fagio wa Raba(Mopper) | |
| 7 | Jembe lenye Mpini | |
| 8 | Fyekeo na Reki | |
| 9 | Ream (A4) ya karatasi mbili (2) kwa mwaka | |
| 10 | Folder file 2 (Kwa Taarifa Zake) | |
| 11 | **Nakala ya Hati ya matokeo (Result Slip)** | |

Michango yote ya Shule inatakiwa kulipwa kupitia **Benki ya NMB** kwa **Namba ya Akaunti – 50901100037 Jina la Akaunti – CHOMASECONDARY SCHOOL REC A/C**.

**KUMBUKA KUANDIKA JINA LA MWANAFUNZI KWENYE KARATASI YA BENKI YA MALIPO**, Mwanafunzi lazima *alete fomu aliyotumia kuweka fedha Benk* ***(Bank Pay in Slip)*** inayoonesha umelipa michango hiyo, jina la mwanafunzi pamoja na kidato anachosoma vinapaswa kuonekana katika hiyo ***Bank Pay in Slip***. Fuata maelekezo ya mchanganuo wa malipo elekezi hapo juu na *michango ambayo haijaelekezwa kulipia Bank*

*Hakikisha unakuja nayo shuleni na si vinginevyo.*

**MAHITAJI MENGINEYO**

1. Mwanao aje na picha za rangi 4 (passport size) zipigwe akiwa amevaa sare ya shule nyuma kitambaa kiwe cha rangi ya blue.
2. Daftari 10 (Counter book - Quire 4) kwa idadi ya tahasusi yake aliyochaguliwa pamoja na kalamu za kutosha.
3. T – shirt ya shule 2 (Shamba Dress), T-shirt hizo zinapatikana Shule kwa gharama ya Tsh 10,000/= @ 1
4. Mwanao aje na vitabu bora kwa kila somo, kwa masomo ya tahasusi yake. (orodha imeambatanishwa ukurasa wa mwisho kwenye fomu hii)
5. Aje na **scientific calculator** (**fx-991MS**), **CASIO** "Iwe ni Non Programmable Calculator" kwa tahasusi za PCM, PCB na CBG
6. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biolojia.
7. **AFYA:** Mzazi unatakiwa kumkatia mwanao **BIMA YA AFYA** (Bima Kubwa ya NHIF) kwa ajili ya matibabu kwa mwaka

## B: SARE YA SHULE YA SEKONDARI CHOMA.WAVULANA

1. Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi (Tetron).
2. Suruali mbili (2) za rangi ya **BROWN (kahawia)** **zisizobana kitambaa kiwe kizito (E-stim 1)** kulingana na urefu wako yenye marinda mawili kila mguu na iwe na upana wa kutosha (***isiwe modal***). Upana

wa chini usipungue 20cm, ukunjwe kwa pindo la nje (*TurnUp)*. Isiwe ya kubana na mifuko yake iwe ya pembeni, siyo ya mbele aina ya (*Pisto)*.

3. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga Kamba visivyo na madoido yoyote jozi mbili. (Sio buti)
4. Aje na soksi nyeusi jozi mbili.
5. Sweta moja la mikono mirefu, rangi ya kijivu yenye nembo ya Shule.
6. Suruali mbili **Damu ya mzee** (Shamba Dress) ambazo huvaliwa wakati wa masomo ya jioni au kazi za jioni.

**WASICHANA**

1. Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi yasiyo na maua, yasibane mwili (Tetron / Tomato). Shati ichomekewe ndani ya sketi wakati wote.
2. Sketi mbili za rangi ya **BROWN (kahawia)** **(kitambaa kiwe kizito, E-stim 1)** zenye marinda 14 (Kumi na nne) ya kupanga, ziwe zinavuka magoti,(inchi 8 kutoka usawa wa goti), **ZISIZOBANA MWILI**.
3. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vyenye kutumia kiwi na sio petrol vyenye visigino vifupi.
4. Soksi ndefu nyeupe jozi mbili.
5. Sweta moja la mikono mirefu, rangi ya kijivu yenye Nembo ya Shule.
6. Sketi mbili **Damu ya mzee** (Shamba Dress) ambazo huvaliwa wakati wa masomo ya jioni au kazi za jioni.
7. Wasichana wa ***Kiislamu wanaopenda kuvaa Hijabu wakati wa masomo wanaruhusiwa*** lakini **hijabu iwe ya kushona nyeupe** isiwe ya dukani, **Nusu kanzu nyeupe isiyobana** na sketi ndefu ya **BROWN (Kahawia)** yenye ***Rinda box*** moja mbele na moja nyuma.

## C: VIFAA VYA BWENI NA MALAZI.

1. Aje na shuka mbili (2) rangi ya light blue na pinki.
2. Aje na godoro futi mbili na nusu kwa sita.
3. Aje na Chandarua cha pande nne na siyo cha mviringo kwa juu cha kuzuia mbu.
4. Aje na Ndoo mbili zenye ujazo wa lita kumi (10)
5. Aje na ndala jozi moja kwaajili ya kuogea pamoja na Taulo.
6. Aje na mswaki na dawa ya meno, sabuni ya kuogea na kufulia za kutosha muhula mzima,toilet paper 5.
7. Aje na taa moja ya betri au solar ambayo ataitumia wakati umeme unapokatika.
8. Aje na sanduku imara la bati pamoja na kufuli kwaajili ya kuhifadhia vitu vyake vyote.
9. Aje na kiwi nyeusi na brashi ya viatu.
10. Aje na Dumu 1 la lita 5 kwaajili ya kuhifadhia maji ya kunywa.

## D. VIFAA VYA CHAKULA

Aje na;-

1. Sahani yenye Vyumba-vyumba ya Chuma (Aluminum tray), kikombe cha Plastiki kimoja na kijiko tu!

## E. VIFAA VYA MICHEZO

**Aje na;-**

1. T-shirt mbili (2) za rangi ya Blue
2. **Kwa Wasichana**, aje na Sketi mbili (2) za *Damu ya mzee*. Ashone kwa kufuata maelekezo kama yale ya sketi za Brown (Kahawia) (kitambaa kizito malinda (14) inchi 4 kutoka usawa wa goti kwa kwenda chini. ***Kwa wanafunzi wa kiisilamu aje na Sketi ndefu ya Damu ya mzee yenye linda box moja mbele pamoja na Hijabu ya Kijivu na nusu kanzu yake yenye rangi ya kijivu.***
3. **Kwa Wavulana,** Suruali mbili za rangi ya *Damu ya mzee* zishonwe kwa kufuata maelekezo ya suruali ya Brown(Kahawia).
4. Raba za kuvaa wakati wa michezo, kazi na wakati wa masomo ya jioni ni rangi yoyote.
5. Track suit moja (1), rangi ya kijivu.
6. Bukta moja (1) ya rangi ya blue

**FOMU NAMBA 2.**

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI.**

1. (a) Jina la mwanafunzi_________________________________(b) Anuani _________________

2. Tarehe ya kuzaliwa __________________________

3. Shule aliyomalizia darasa la saba__________________________Mwaka __________________

4. Mkoa anaotoka______________________Wilaya alipozaliwa ____________________

5. Tarafa anayotoka_______________________Kata atokayo _______________________

6. Kijiji anachotoka_______________________Mtaa / kitongoji anaotoka ______________________

7. Jina la Mtendaji wa (a) Kata______________________(b) Mtaa/Kijiji _______________________

9. Jina la (a) Balozi wa nyumba kumi ________________________________________

(b) Mwenyekiti wa Mtaa ___________________________________________

10. Michezo anayopendelea

| **Na.** | **Jina la Mchezo** |
|---|---|
| 1. | |
| 2. | |
| 3. | |
| 4. | |
| 5. | |

11. Nafasi yoyote ya uongozi aliyowahi kushika

| **Na.** | **Aina ya Uongozi** | **Shule** | **Mwaka** |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |
| 4. | | | |
| 5. | | | |

Nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa hapo juu ni za kweli, pia nathibitisha kuwa nitakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi pamoja na kuwa na bidii ya masomo na sitapata chini ya alama 70 chini ya 100 kwa kila mtihani,zoezi au jaribio nitakalofanya hapa shuleni.

**Jina la Mwanafunzi______________________________Sahihi________________Tarehe ___________**

**FOMU NAMBA 3.**

**TAARIFA ZA MZAZI WA MWANAFUNZI AU MLEZI:**

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi ______________________________________________
2. Kazi anayofanya mzazi __________________________________
3. Anuani ________________________________
4. Namba ya simu_____________________________________(inayopatikana muda wote)
5. Mkoa_____________________Wilaya_______________Tarafa_________________

   Kata______________________Kijiji________________Mtaa __________________
6. Anuani kamili ya nyumbani ambako mwanafunzi atakuwa anakwenda wakati wa likizo

Mahali________________________________Kwa nani__________________Nyumba Na: ______

7. Majina ya viongozi/Wazazi /walezi atakakokuwa anakwenda wakati wa likizo:

   Jina la Baba /mlezi/ndugu _____________________________________

   Jina la mama/mlezi __________________________________________

   Jina la Mtendaji wa Kata anakoishi mzazi / wazazi ______________________________

   Jina la Mtendaji wa Kijiji/Mtaa anakoishi mzazi / wazazi _________________________

   Jina la Mwenyekiti wa Mtaa / kitongoji anakoishi mzazi / wazazi __________________________

   Balozi wako wa nyumba kumi _____________________________________

Mimi Mzazi/Mlezi wa_______________________________________ninaahidi kushirikiana na walimu pamoja na watumishi wote wa Shule ya Sekondari **CHOMA** katika kumlea mwanangu kwa muda wote atakapokuwa hapa shuleni **CHOMA** Sekondari.

Nitaomba kujulishwa mara moja endapo mwanangu ameenda kinyume na sheria, kanuni na taratibu za shule. Pia nitakuwa tayari mwanangu kupewa adhabu inayostahili kwa makosa atakayofanya. Ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule pale itakapobidi.

**Jina la Mzazi/Mlezi_____________________________Sahihi_____________Tarehe _______**

**NB. Mzazi/ Ndg. ambaye picha yake haipo hapa chini katika fomu hii haruhusiwi Kuja kumwona au kumtembelea mwanafunzi hapa Shuleni.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **PICHA NA.1** | **PICHA NA.2** | **PICHA NA.3** | **PICHA NA.4** |

**FOMU NAMBA 4.**

**YAH: KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KWAMWAKA WA MASOMO WA 2023 / 2024**

**1.0 Mimi** _______________________________________________ nimepokea barua ya kuchaguliwa kujiunga na Kidato cha **TANO** katika Shule ya Sekondari Choma. **NIMEKUBALI / NIMEKATAA** nafasi hii (ondoa kati ya neno NIMEKUBLI AU NIMEKATAA kwa kulikata na kalamu ya blue / nyeusi) baada ya kusoma na kuelewa yaliyoandikwa katika fomu na barua ya kujiunga.

Ninaahidi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu kuwa nikishafika shuleni, nitazingatia kanuni, sheria na taratibu zote za shule kwa kipindi chote cha mimi kuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Choma. Na nimeelewa kanuni na taratibu zote za shule na sitajihusisha na vitendo vya uvunjaji wa amani shuleni, kushiriki kufanya fujo, vurugu, migomo, kuvuta bangi na matumizi ya madawa ya kulevya pamoja na makosa ya jinai.

Nitatumia juhudi na maarifa katika kujiendeleza kwa manufaa yangu na Taifa kwa ujumla.

**Jina la mwanafunzi** _________________________________ **Sahihi** ______ **Tarehe** ___________

**Jina la Mzazi/Mlezi** _______________________________**Sahihi** ___________**Tarehe** ___________

**2.0 Sheria na kanuni za Shule ya Sekondari Choma**

2.1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewana Wizara zenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni:-

(a) Heshima kwa walimu, viongozi, wazazi, wafanyakazi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni lazima.
(c) Kuhudhuria vipindi vyote darasani na kuudhuria mitihani yote inayofanyika shuleni ikiwemo Majaribiokulingana na **TAHASUSI** yako.
(c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa ni lazima.
(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati woteukiwa mwanafunzi wa shule hii.
(e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule ni lazima.
(f) Kuvaa sare ya shule wakati wote utakapotakiwa na kuzingatia ratiba ya shule ni lazima.

2.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule mara moja.

1. Wizi.
2. Uasherati na ushoga.
3. Ubakaji.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k
5. Kupigana na kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau Bendera au Nembo ya Taifa.
8. Kuoa au kuolewa.
9. Kupata, kusababisha au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.
10. Kugoma, kuchochea, kuongoza au kushiriki migomo au kuvunja amani na usalama wa shule au watu.
11. Kukataa adhabu kwa makusudi.
12. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shuleni.
13. Kukaidi maagizo ya shule.

**NB: AFIKE AKIWA AMEVAA SARE ZA SHULE (NGUO ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIWI)**

**FOMU NAMBA 5.**

**To the Medical Officer**

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF MR/MISS**

______________________________________________________

Please examine the above named pupil and give us the report regarding his/her suitability for undertaking secondary school students.

1. Student full name______________________________________age ________________
2. Blood ________________________________________________________
3. Stool ________________________________________________________
4. T.B. Test ____________________________________________________
5. Syphilis Test _________________________________________________
6. Urine Examination _____________________________________________
7. Eye Test _____________________________________________________
8. Chest Test ____________________________________________________
9. Ears Test _____________________________________________________
10. Spleen ______________________________________________________
11. Abdomen _____________________________________________________

ANY ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical defects or impairment, infection, family diseases etc.

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

I certify that, the above pupil is suitable/unsuitable for secondary school students. If unsuitable give reasons:

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

Name of **Medical Officer**:__________________________________Signature __________________

Date: ___________________________________ Official stamp:

## ZINGATIA:

(i) Tafadhali, mwanao asome sheria, kanuni na taratibu za shule na kama yuko tayari kufuata taratibu husika akiri mbele yako kwa kujaza fomu husika zilizoambatanishwa.

(ii) Mwanafunzi atakae chelewa kufika shuleni zaidi ya tarehe **30 / 08 / 2023** hatapokelewa. Hivyo ni vyema ukamwandaa mapema mwanao na akafika mapema shuleni. Wanafunzi wa kidato cha tano wataanza kuingia darasani na kufundishwa tarehe **14 / 08 / 2023**

**(iii) Mwanafunzi awapo shuleni haruhusiwi kumiliki simu. Iwapo mwanafunzi atabainika / atakamatwa na simu atasimamishwa au ikibidi atafukuzwa shule**

**TAFADHALI, MWANAO AFIKE SHULENI NA BARUA HII NA AJAZE KWA UKAMILIFU SEHEMU YA TAARIFA MAALUM KWA MWANAFUNZI ANAYEANZA KWA MARA YA KWANZA.**

Nakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja CHOMA SEKONDARI.

*KARIBU SANA*

William Emidi Augustine
**MKUU WA SHULE**

***NB: Kwa maelezo ya ziada Ukipata Changamoto yoyote tafadhali wasiliana na wafuatao:-***

- MAKAMU MKUU WA SHULE 0768843830
- MWANDAMIZI TAALUMA 0788169196 / 0769078009
- MWANDAMIZI MALEZI 0764678194 / 0769585806
- MHASIBU WA SHULE 0762338455 / 0784287072 / 0713377143

**ORODHA YA VITABU KWA KILA TAHASUSI ( COMBINATION )**

**1. GENERAL STUDIES FOR ADVANCED LEVEL BY**

- BIGIRWAMUNGU
- RICHARD MBALASE
- NYAMBARI NYANGWINE.

GS QUESTIONS AND ANSWERS.

**2. PHYSICS REFERENCE BOOKS**

1 . Cand, S (2008) Principles of Physics for Class XI & XII, New Delhi. 2 . Duncan, T, New Understanding Physics for A-level.

3. Muncaster. R, ( 1993 ) *A – LEVEL PHYSICS 4th Ed*, Nelson Thornes Ltd, U. K.
4. Mehta . v. k, ( 2013 ) *S.Chand's Principles of PHYSICS for Class XII 7th ED*
5. *. Nelkon & Parker (1995) Advanced Level Physics 7th Edition. Longman International Education.*

**3: CHEMISTRY REFERENCE BOOKS**

1. Jain. S.K, (2010), *Conceptual chemistry For Class x1*, S. Chand & Company Ltd, New Delhi, India.
2. Mkayula, L.L et al (1998), *Phyisical Chemistry*, *Volume 1*, (Mzumbe Book Project), Mzumbe, Tanzania.
3. Bahl. B.S et al (2009), *Essentials of Physical Chemistry*, S. Chand & Company Ltd, New Delhi, India.
4. Ramsden. E.N, (2000), *A – Level Chemistry, 4th Ed*, Nelson Thornes Ltd, U.K.

**4: BIOLOGY REFERENCE BOOK.**

(i) Taylor D.J, (1999), *Biological Science*, 3rd Ed, Cambridge University Press London.

(ii) Susan Toole – Understanding Biology

(iii) Msaki, L (2003) Cell Structure.

(iv) Msaki L (2003) Systematics and Classification.

**5: ADVANCED MATHEMATICS REFERENCE BOOKS**

1. Horril. P. J.F. ( 1985 ) , *Pure Mathematics Book 2, 3rd Ed*, Longman Group Limited, London.
2. Tranter . C. J. ( 1975) , *ADVANCED LEVEL PURE MATHEMATICS*, *4th Ed,*Hodder& Stoughton, London.
3. Dass . H. K & Verma, R. ( 1997 *) S. CHAND'S MATHEMATICS FOR CLASS XII* (VOLME II), S.CHAND & COMPANY LTD. New Delhi.
4. Hume. H. ( 1975 ) , *An Introduction to Probability and Statistics, Revised Ed,* University of Western Australia Press, Western Australia.